

# COMPETENCE BASED CURRICULUM

D003

MONITORING LEARNER'S PROGRESS

GREDI YA TANO - MWAKA 2022

[5]

KISWAHILI

Jina: .....

Nambari ya Mwanafunzi :

Jinsia: Mvulana  Msichana

Jina la Shule: .....

Kuzidisha matarajio	Kufikia matarajio	Kukaribia matarajio	Mballi na matarajio

## SEHEMU YA A

### ZOEZI LA 1 : KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

(alama 5)

1. Mwalimu amsalimie mwanafunzi kisha amuilize maswali yafuatayo.

- Unda maneno mawili yanayoanzia na sauti 'ah'
- Taja salamu moja na jibu lake.
- Tunga sentensi ukitumia maneno 'niwle radhi'
- Tegua kitendawili: Nariywa supu natupa nyama.

### ZOEZI LA 2: KUSOMA KWA SAUTI




2. Soma kifungu hiki kwa sauti.

(alama 10)

Ulikuwa ni wakati wa likizo ya mwezi wa Disemba. Nilikuwa na furaha nyingi sana kwani nilikuwa nimepita vizuri kwenye mihani wangu wa mwisho wa muhula. Babangu alikuwa ameniahidi kuninunulia baiskeli. Hivyo basi, nilifurahi zaidi alipoamua kutimiza chadi yake. Siku moja, aliamka na kujitayarisha. Alinambia kuwa tungeenda sokoni akaninunulia baiskeli. Nilijiandaa kwa haraka kisha tukaondoka nyumbani. Sokoni, tulilitafuta duka lililokuwa likiuzua baiskeli. Alinunua baiskeli moja kisha akapewa risiti. Tulirudi nyumbani huku nikiwa mwenye furaha zaidi. Nilimshukuru babangu sana. Nami nilimuahidi kuwa ningeendelea kutia bidii zaidi shuleni.

SEHEMU YA B

ZOEZI LA 3: SARUFI

3. Pigia mstari vihusishi katika sentensi zifuatazo. (alama 4)
- (a) Wasafiri walingojea matwana kando ya barabara.  
(b) Mti umemea karibu na nyumba.  
(c) Aliyatia maji ndani ya chungu.  
(e) Ndege alitua juu ya mti.
4. Andika kinyume cha neno lililopigiwa mstari. (alama 3)
- (a) Mjakazi alianika nguo uani. \_\_\_\_\_  
(c) Mtoto aliwasha moto kimakosa. \_\_\_\_\_  
(d) Yingo alipakia mizigo. \_\_\_\_\_
5. Andika majina ya maumbo yafuatayo. (alama 3)
- (a)  \_\_\_\_\_
- (b)  \_\_\_\_\_
- (c)  \_\_\_\_\_
6. Kanusha sentensi zifuatazo (alama 2)
- (a) Wewe utapewa tuzo. \_\_\_\_\_  
(b) Maria ataenda shuleni. \_\_\_\_\_  
(c) Watoto wanacheza uwanjani. \_\_\_\_\_
7. Andika maneno yaliyo kwenye ngeli hizi. (alama 3)
- (a) A - WA \_\_\_\_\_  
(b) LI - YA \_\_\_\_\_  
(c) I - ZI \_\_\_\_\_  
(d) KI - VI \_\_\_\_\_

8. Andika sentensi hizi katika wakati ullopita.

(alama 3)

(a) Mama ameenda sokoni. \_\_\_\_\_

(b) Baba analima kondeni. \_\_\_\_\_

(c) Wanafunzi wataimba wimbo mpya. \_\_\_\_\_

9. Jaza pengo kwa kutumia kiambishi mufti.

(alama 4)

(a) Ukuni \_\_\_\_\_ liochomwa ni huu.

(b) Nguo \_\_\_\_\_ takazofuliwa ni chafu.

(c) Chupa \_\_\_\_\_ iliyovunjika ni yangu.

(d) Vikapu \_\_\_\_\_ livyoshonwa ni hivi.

#### ZOEZI LA 4:UFAHAMU

10. Soma hadithi kisha ujibu maswali yafuatayo.

(alama 5)

Hapo zamani za kale, nyoka na jongoo walikuwa wasena wakuu. Walisaidiana kwa vyovyote vile. Shida ya mmoja ilikuwa ya yule mwingine. Hata hivyo, bada ya miaka mingi katika urafiki wao, jongoo alianza kumwonea nyoka wivu kwa sababu nyoka alikuwa na miguu ilhali jongoo hakuwa nayo. Alipanga njama ya kumhadaa ili amnyang'anye miguu yake. Alimwenda nyoka pale pangoni na kumwomba, "mwenzangu nyoka, nimealikwa kwenye sherehe ya binti yangu lakini nina tatizo moja. Sina miguu ya kunifikisha huko. Niazame miguu yako, nami nikirudi nitakurudishia." Nyoka hakusifa. Kwa kuwa walipendana sana, alimuazima rafikiye miguu yake ili aende shereheni. Alipoondoka, nyoka alisalia pale pangoni akingojea miguu yake lakini aliambulia patupu. Jongoo alichukua miguu ya nyoka kilazima na akaitumia kuenda nchi za mbali. Nyoka alilia kwa uchungu mwingi lakini maji yakimwagika hayazoleki. Hadi leo, nyoka hutembea kwa tumbo kwa sababu hana miguu.

(a) Neno 'wasena' kwenye hadithi lina maana ya \_\_\_\_\_

(b) Kwa nini jongoo alimwonea nyoka wivu?  
\_\_\_\_\_

(c) Nia ya jongoo kupanga njama ilikuwa ni \_\_\_\_\_

(d) Kulingana na hadithi, jongoo alihitaji miguu ili \_\_\_\_\_

(e) Maneno "maji yakimwagika hayazoleki" ni mfano wa  
\_\_\_\_\_

